**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI - KAMPASI KUU DODOMA**

# FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA STASHAHADA KWA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA NA TAMISEMI (DIPLOMA-3 YEARS) KWA MKUPUO WA SEPTEMBA KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027.

Mkuu wa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (Institute of Rural Development Planning) anawapongeza wanafunzi wote waliochanguliwa na TAMISEMI kujiunga katika kozi mbalimbali na kuwakaribisha wahitimu wote wa kidato cha nne wenye sifa ya kujiunga na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

Kwa wale ambao hawajachaguliwa na TAMISEMI wanaweza kutuma maombi ya mkupuo wa **SEPTEMBA** moja kwa moja chuoni kwa njia ya mtandao kupitia oas.irdp.ac.tz

**Kozi zinazotolewa kwa ngazi ya Stashahada (Diploma-3 Years) ni:**

i. Stashahada katika Mipango ya Maendeleo Vijijini (Diploma in Rural Development Planning).

ii. Stashahada katika Utawala na Usimamizi wa Maendeleo (Diploma in Development Administration and Management).

iii. Stashahada katika Maendeleo ya Jamii (Diploma in Community Development)

iv. Stashahada katika Upimaji Ardhi na Ramani (Diploma in Geomatics)

v. Stashahada katika Mipango Miji na Vijiji (Diploma in Urban and Regional Planning)

vi. Stashahada katika Uhasibu na Fedha (Diploma in Accounting and Finance)

vii. Stashahada katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Diploma in Information and Communication Technology)

viii. Stashahada katika Usimamizi wa Ardhi na Uthamini (Diploma in Land Management and Valuation)

ix. Stashahada katika Takwimu (Diploma in Statistics)

x. Stashahada katika Uchumi (Diploma in Economics)

xi. Stashahada katika Sheria (Diploma in Law)

**Sifa za Mwombaji:**
Mwombaji awe amehitimu **KIDATO CHA NNE** na kufaulu angalau kwa alama “D” katika masomo manne yoyote isipokuwa masomo ya dini au awe amehitimu astashahada ya msingi na kufaulu kwa kiwango cha “GPA ya 2.0 au zaidi” katika programu zinazoendana. Kwa waombaji wa Stashahada ya Upimaji Ardhi na Ramani wanatakiwa kuwa na ufaulu wa angalau alama “D” kwa somo la Jiografia, Hisabati au Fizikia katika matokeo ya **KIDATO CHA NNE** au awe amehitimu astashahada ya msingi ya Upimaji Ardhi na Ramani na kufaulu kwa kiwango cha “GPA ya 2.0” au zaidi.

**Muda wa Masomo:**

- Masomo ya Stashahada hutolewa kwa muda wa miaka mitatu kwa mjumuisho wa mafunzo ya nadharia na vitendo.

**ZINGATIA 1**: Mwanafunzi aliyejiunga kutokea **KIDATO CHA NNE** anatakiwa asome ngazi ya astashahada ya msingi (Basic Technician Certificate) mwaka wa kwanza wa masomo. Mwanafunzi huyu akipata ufaulu wa “GPA ya 2.0 au Zaidi” atatakiwa aendelee na mwaka wa pili wa masomo katika ngazi ya astashahada (Technician Certificate) ambayo akifaulu kwa “GPA ya 2.0 au Zaidi” atatakiwa kuendelea na mwaka wa tatu wa masomo katika ngazi ya stashahada (Ordinary Diploma)

**ZINGATIA 2**: Mwanafunzi aliyejiunga kutokea **ASTASHAHADA YA MSINGI (BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE)** anatakiwa asome miaka miwili kwa kuanza na ngazi ya astashahada (Technician Certificate) mwaka wa kwanza wa masomo. Mwanafunzi huyu akipata ufaulu wa “GPA ya 2.0 au Zaidi” katika ngazi aliyoingia nayo atatakiwa aendelee na mwaka wa pili wa masomo katika ngazi ya stashahada (Ordinary Diploma)

**Kuripoti Chuoni**
Wanafunzi watapaswa kuripoti Chuoni tar **19/10/2026** na kuwasili na vitu vifuatavyo

**i. Vyeti vya masomo**

Mwanafunzi wanapaswa kuwasili na vyeti halisi (original certificates) vya Taaluma na cha kuzaliwa (Zingatia: Chuo kitapokea nakala halisi ya matokeo “valid results slip” kwa waliomaliza 2025 tu)

## ii. Ada ya Masomo (Tution Fee) na Michango ya moja kwa moja (Direct Cost) ya Mwaka wa Kwanza wa Masomo kwa wanafunzi walihitimu KIDATO CHA NNE

- ADA YA MASOMO (TUITION FEE) kwa kozi zote za stashahada (Diploma) isipokuwa kwa kozi za kada ya Upimaji Ardhi, Mipango Miji na Vijijini (Urban and Regional Planning), na Usimamizi wa Ardhi na Uthamini (Land Management and Valuation) ni TZS 830,000/=

- ADA YA MASOMO (TUITION FEE) kwa kozi za Astashahada ya Msingi ya Upimaji Ardhi (Geomatics), Mipango Miji na Vijiji (Urban and Regional Planning) na Astashahada ya msingi katika Usimamizi wa Ardhi na Uthamini (Land Management and Valuation) ni TZS 905,000.00/=

**Jedwali Na. 1** Mchanganuo wa Michango ya Moja kwa Moja (Direct Cost) = 335,000/= (Malipo aya yanalipwa mara moja pindi mwanafunzi anaporipoti chuoni (Wakati wa Usajili)

| | |
|---|---|
| Gharama ya kutuma maombi (Application Fee) | TZS 15,000.00/= |
| Gharama ya usajili (Registration Fee) | TZS 60,000.00/= |
| Gharama ya kitambulisho (Identity Card) | TZS 10,000.00/= |
| Gharama ya huduma ya serikali ya wanafunzi (Student Organization Fee) | TZS 20,000.00/= |
| Gharama ya huduma za michezo (Sports and games Fee) | TZS 10,000.00/= |
| Gharama ya uthibiti ubora wa NACTVET (NACTVET Quality Assurance Fee) | TZS 20,000.00/= |
| Gharama ya mitihani (Examination fee) | TZS 30,000.00/= |
| Gharama ya huduma ya mtandao (Internet fee) | TZS 10,000.00/= |
| Gharama ya huduma ya maktaba (Library services Fee) | TZS 10,000.00/= |
| Gharama ya Maandalizi ya kuhitimu (Graduation fee) | TZS 50,000.00/= |
| Gharama ya cheti (Transcript Fee) | TZS 20,000.00/= |
| Gharama ya huduma za kompyuta (Computer lab fee) | TZS 40,000.00/= |
| Gharama ya uratibu wa mafunzo kwa vitendo (Field supervision) | TZS 40,000.00/= |

**Jedwali Na. 2:** Mchanganuo wa namna ya ulipaji wa ada ya masomo na michango ya moja kwa moja (Direct Cost) kwa kozi zote za stashahada (Diploma) isipokuwa kwa kozi za kada ya Upimaji Ardhi, Mipango Miji na Vijijini (Urban and Regional Planning), na Usimamizi wa Ardhi na Uthamini (Land Management and Valuation)

| | Siku ya kuripoti | Kabla ya Majaribio ya Pili (Test II) | Kabla ya Mitihani ya Muhula | Jumla kwa Muhula |
|---|---|---|---|---|
| Muhula wa Kwanza | TZS. 335,000.00 | TZS. 215,000.00 | TZS. 200,000.00 | TZS. 750,000.00 |
| Muhula wa Pili | TZS 215,000.00 | TZS. 100,000.00 | TZS 100,000.00 | TZS. 415,000.00 |
| | Jumla Kuu kwa Mwaka | | | TZS. 1,165,000.00 |

**Jedwali Na. 3:** Mchanganuo wa ada kwa kozi za Astashahada ya Msingi ya Upimaji Ardhi (Geomatics), Mipango Miji na Vijiji (Urban and Regional Planning) na Astashahada ya msingi katika Usimamizi wa Ardhi na Uthamini (Land Management and Valuation)

| | Siku ya kuripoti | Kabla ya Majaribio ya kwanza (Test II) | Kabla ya Mitihani ya Muhula | Jumla kwa Muhula |
|---|---|---|---|---|
| Muhula wa Kwanza | TZS. 335,000.00 | TZS. 252,500.00 | TZS. 200,000.00 | TZS. 787,500.00 |
| Muhula wa Pili | TZS 252,500.00 | TZS. 100,000.00 | TZS 100,000.00 | TZS. 452,500.00 |
| | Jumla Kuu kwa Mwaka | | | TZS. 1,240,000.00 |

**iii. Mahitaji mengine**

a. Bima ya afya TZS. 50,400/= (Malipo haya yatafanyika na wanafunzi wote ambao hawana bima ya afya kutoka NHIF inayofanya kazi)

b. Gharama ya vipimo vya afya TZS. 5000/= (Vipimo vinafanyika kwenye Zahanati ya Chuo na malipo yatafanyika mara moja wakati wa usajili)

c. Gharama ya hosteli TZS. 350,000/= kwa Mwaka (Malipo haya yatalipwa mara moja kwa mwaka kwa wale watakaopenda kukaa ndani ya hosteli za chuo).

iv. Malipo yote yatafanyika kwa kupitia **CONTROL NUMBER** zitakazotolewa kwenye mfumo wakati wa usajili

v. Wanafunzi watajigharamia gharama za chakula, shajala (stationary) na kujikimu wakati wamafunzo ya vitendo

vi. Chuoni hakuna sare, ila wanafunzi wanapaswa kuvaa mavazi yanayokubalika kwa mujibu wa miongozo na taratibu za serikali.

**Kwa msaada na maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi:**
Kampasi kuu Dodoma: 0746 777 001, 0746 777 002, 0746 777 003, 0746 777 006, 0746 888 063, AU 0744 254305
**Imetolewa Na:**
**Kurugenzi ya Huduma Saidizi za Taaluma**
**Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini-Kampasi Kuu Dodoma**